



# **NENO KUTOKA KWA MWENYEKITI WA BARAZA LA MASHIRIKA YASIYOKUWA YA KISERIKALI (NACoNGO) KATIKA MKUTANO WA MAJADILIANO YA KIMKAKATI**

**KATIKA UKUMBI WA BENKI KUU-DAR ES SALAAM.**

**TAREHE 09. 02. 2024**

**Waheshimiwa Mawaziri,  
Viongozi mbalimbali wa Serikali mlioko hapa,  
Wadau wa Maendeleo,  
Washiriki wote wa kongamano hili,**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA!**

Kipekee kabisa napenda kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa kuandaa kongamano hili muhimu la kimkakati kati ya Serikali na wadau wa Maendeleo. Sisi kama Baraza la Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali (NaCoNGO) tunaendelea kutoa shukrani na kuipongeza Serikali kwa kutambua mchango wa Asasi za Kiraia na kuzipa nafasi ya ushiriki katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya taifa kwa manufaa mapana ya watanzania na kuhakikisha kwa pamoja tunapeleka mbele maendeleo ya taifa kwa ujumla. Nitoe shukrani kwa wadau wote wa maendeleo ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia na wamekuwa sehemu ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo.

Katika maandalizi yanayoendelea ya kuandaa **Dira** ya maendeleo – 2050, sisi wana AZAKI tumeanza kutoa mchango wetu katika kuhakikisha **Dira** hiyo inazingatia suala zima la maendeleo jumuishi, hususani ushiriki wa makundi maalum katika shughuli za kiuchumi na huduma za jamii unapewa kipaumbele katika utekelezaji wa afua mbalimbali za serikali na wadau wake.

Katika mjadala wa leo, tutachangia maoni yetu juu ya uwekezaji katika rasilimali watu kwa mtazamo wa maendeleo jumuishi, ukuaji wa kilimo na usalama wa chakula, hali ya miundomsingi wezeshi katika maeneo ya vijijini na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa makundi maalumu.

## **MADA YA KWANZA**

*Uwekezaji katika rasilimali watu kwa mtazamo wa maendeleo jumuishi (Human Capital Development)*

### **Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Maendeleo,**

Uwekezaji katika rasilimali watu ni afua namba moja katika maendeleo ya nchi yoyote duniani. Kwa **msingi huo** wana AZAKI tunatoa wito wa kuzingatia azimio la Dar es salaam la mwaka 2023 ambalo linatambua kwamba watu ndio rasilimali muhimu zaidi kwa Bara la Africa hivyo hakuna muda wa kupoteza.

## **MADA YA PILI**

*Ukuaji wa kilimo na usalama wa chakula (Food Systems Strengthening)*

### **Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Maendeleo,**

Wana AZAKI tunapenda kukumbusha na kuisitiza kwamba, sekta ya kilimo bado ni UTI wa mgongo wa uchumi na maendeleo ya taifa hususani katika hukakikisha usalama wa chakula. Hivyo sekta hiyo hainabudi kupewa kipaumbele katika **Dira** ya maendeleo ya 2050.

## **MADA YA TATU**

*Hali ya miundomsingi wezeshi katika maeneo ya vijijini ( Infrastructure development for Increasing productivity)*

### **Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Maendeleo,**

Sisi wana AZAKI tunatambua na kupongeza juhudi za serikali katika ujenzi wa miundomsingi kwa ajili ya shughuli za maendeleo, hususani miundo msingi ya kimkakati. Hata hivyo bado juhudi kubwa zinahitajika katika kuhakikisha miundomsingi hiyo inaelekezwa maeneo ya vijijini, ambako zaidi ya asilimia 60 ya watanzania wanaishi, ili kufungua fursa za kiuchumi kwa maendeleo jumuishi.

## **MADA YA NNE**

*Upatikanaji wa rasilimali fedha kwa makundi maalumu. (Financing for Development)*

### **Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Maendeleo,**

Wana AZAKI tunapenda kukumbusha kwamba bado upatikanaji wa mikopo nafuu kwa shughuli za kiuchumi na uzalishaji mali za makundi maalum bado ni changamoto. Kwa hiyo ni muhimu kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa rasilimali fedha kwa makundi hayo muhimu ili ndoto ya maendeleo jumuishi iweze kutimia.

### **Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Maendeleo,**

Licha ya mchango na jukumu la Sekta ya AZAKI katika jamii, sekta hii bado inaendelea kukabiliwa na changamoto nyingi hasa zile zitokanazo na Mifumo, Sera na Utekelezwaji wa Sheria mbalimbali zinazopunguza ufanisi wake. **TUNAIOMBA SERIKALI IANGALIE UPYA MIFUMO, SERA NA SHERIA HIZO ILI KUONGEZA TIJA KATIKA MCHANGO WA SEKTA YA AZAKI KATIKA KUCHOCHEA MAENDELEO YA TAIFA**

**WAHESHIMIWA MAWAZIRI NA WADAU WA MAENDELEO,  
AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA,**

**Naomba Kuwasilisha.**

**Lilian Badi**

**Mwenyekiti wa Baraza**

**NaCoNGO**